# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI
## HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA
## SHULE YA SEKONDARI NANSIMO
**S.L.P 316 BUNDA, TEL 255-769959007, EMAIL** nansimoss@gmail.com

**KUMB NA HDN/S.636/V.1/2026**

**Namba za simu**

**Mkuu wa shule 0769959007**

**Makamu mkuu wa shule 0757350240**

Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ………………………………………………..

S.L.P ………………………………

……………………………………

YAH**; MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATI SHULE YA SEKONDARI NANSIMO ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA MKOA WA MARA**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii na atasoma tahasusi ya ……..……

Shule ya Sekondari Nansimo iko umbali wa Km 65 kutoka Bunda mjini na km 6 kutoka makao makuu ya Halmashauri iliyoko kibara kando kando mwa barabara iendayo kisorya. Unatakiwa kupanda gari BUNDA MJINI KWA GHARAMA YA SH 7,000, UNATAKIWA KUSHUKA NANSIMO KIBAO CHA SEKONDARI. Ukiwa kibaoni ingia shuleni kwa kupitia barabara ya shule utatembea kama mita mia mbili kufika shuleni.

Muhula wa kuanza masomo utaanza tarehe **…………….. Unatakiwa kuripoti shuleni siku moja kabla ya tarehe ya kufungua shule.** Ofisi ya Makamu Mkuu wa shule itakuwa wazi kwa mapokezi na usajili ukiwa na:

- "Pay in Slip" moja inayoonesha malipo uliyolipia Benki
- Vifaa ulivyoandikiwa katika fomu hii,na fomu nne zilizo ambatanishwa na kujazwa kwa usahihi ***(fomu iliyojazwa na daktari, fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi, ahadi ya mzazi, fomu ya kukubali masharti ya shule na fomu ya picha za wazazi na ndugu wa karibu wa***

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### WAVULANA

- Suruali mbili nyeusi pana mapajani zenye marinda mawili pande zote, mifuko mitatu (mmoja wa nyuma na miwili ya mbele) zenye upana wa sm 16 miguuni.
- Shati mbili (2) nyeupe za mikono mirefu na zenye mfuko mmoja upande wa kushoto.
- Tai ndefu nyeusi na kibanio chake
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visiwe na shingo ndefu na visiwe na visigino virefu.
- Soksi nyeusi jozi mbili (2) na zisiwe na mistari au madoadoa.
- Sweta rangi ya kijivu (V – Shingoni)
- Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

### Nguo za kushindia

- Suruali moja ya kijivu – ESTEM Na 1, pana mapajani yenye malinda mawili kila upande na mifuko mitatu, nyuma mmoja na miwili mbele yenye upana wa sm 16 miguuni,
- T.Shirt 2 za Rangi ya BLUU yenye ufito mweusi shingoni na mikononi yenye nembo ya shule (Inapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh. 15,000/=) kwa atakayependa

### WASICHANA

- Sketi mbili (2) nyeusi zenye rinda boksi. Mkanda wa sketi usizidi inch 1.5 au sm 4. Sketi ziwe ndefu ziguse visigino vya miguu.
- Shati mbili (2) nyeupe za mikono mirefu na zenye mfuko mmoja upande wa kushoto.
- Tai ndefu nyeusi na kibanio chake
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visiwe na shingo ndefu na visiwe na visigino virefu.
- Soksi nyeupe jozi mbili (2) na zisiwe na mistari au madoadoa.
- Sweta rangi ya kijivu (V – Shingoni) 3
- Rangi ya Hijab (kijuba) ni Nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

## Nguo za kushindia

- Sketi moja ya kijivu – ESTEM Na 1 yenye marinda ya kawaida, iwe ndefu iguse visigino,
- T.Shirt 2 za Rangi ya Bluu yenye ufito mweusi shingoni na mikononi yenye nembo ya shule (Inapatikana kwenye duka la shule kwa Tsh. 15,000/= kwa atakayependa)

## SARE ZA MICHEZO

- Viatu vya michezo (Raba), kwa jinsia zote
- Bukta na Tshirt ya Sky bluu
- Track suit ya dark bluu kwa wote

## Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

- Madaftari kumi (10) counter books (Yanapatikana kwenye duka la shule)
- Ream (A4) ya Karatasi mbili (2) kwa mwaka; ).,Rulled paper Mbili (02) kwa muhula. (vinapatikana kwenye duka la shule)
- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (orodha imeambatanishwa)
- Scientific Calculator kwa tahasusi za EGM, HGE na CBG (zinapatikana kwenye duka la shule)
- Godoro la sponge; upana wa ft 2.5 kwa ft 6. (Yanapatikana kwenye duka la shule)
- Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 na mto 1
- Kanda mbili za kuogea
- Nguo za ndani za kutosha;
- Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
- Ndoo 2 kubwa (lita ishirini) zenye mifuniko;
- Sanduku la bati/mbao kwa ajili ya kutunzia vitu vyake (Ni lazima).
- Dumu la lita 5 la kutunzia maji ya kunywa
- File Folder 1 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake shuleni xiv. Picha nne (4) za passport size akiwa amevaa sare ya shule. (Yanapatikana kwenye duka la shule)
- Bima ya Afya, kwa wale wasiokuwa na bima waje na Tsh: 50,400/= kwa ajili ya kutengenezewa kadi ya bima ya mwanafunzi. (Bima ya afya ni lazima)

**NB. Kwa wale wanafunzi wa tahasusi ya CBG wanatakiwa waje na:-**

**Dissection kit** – Kwa ajili ya upasuaji wa wanyama wadogowadogo katika maabara
**Dissection Tray** – kwa ajili ya kuwekea mnyama anayepasuliwa wakati zoezi la upasuaji likiendelea (CBG).
**Laboratory coat** – Kwa ajili ya kuvaa wakati wa mazoezi ya maabara kuzuia madhara ya kemikali (CBG).
**Gloves box 01**– kwa ajili ya kuvaa wakati wa vipindi vya maabara (kwa wanafunzi wa tahasusi ya CBG tu).
**Mask (balakoa)** box 01- kwa ajili ya kuzuia gesi za sumu wakati wa majaribio maabara (kwa wanafunzi wa tahasusi ya CBG tu).

**VIFAA VYA USAFI**

| SN | TAHASUSI | VIFAA WATAKAVYOLETA |
|---|---|---|
| **1** | **CBG** | SQUIZER, SOFTBROOM |
| **2** | **EGM** | **RAKE 1, JEMBE 1** |
| **3** | **HGE** | **PANGA , HARDBROOM** |
| **4** | **HKL** | **SOFTBROOM, JEMBE 1** |
| **5** | **WOTE** | **DAWA YA CHOONI LITA 5, CHELEWA** |

- **Michango mbalimbali**

Michango ya shule ni kama ifuatavyo

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo kwa sare za darasani tu | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

***Michango yote ilipwe kwenye Akaunti ya shule kwa*** *NO* ***30101200078 NMB na*** *Jina la Akaunti ni* ***Recurrent Account, Nansimo Secondary. Mwanafunzi awasilishe*** *Bank pay slip yenye jina la mwanafunzi tu.*

# SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**Sheria na Kanuni za Shule**

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
- Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
- Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
- Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule; 5 vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
- Kutunza mali za shule;
- Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya uongozi wa shule; na
- Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU**:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali϶ maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).
- Mzazi unashauriwa kumwandalia mtoto wako BIMA YA AFYA϶ ya NHIF na aje nayo kwa ajili ya matibabu awapo shuleni, endapo atakosa bima mzazi atawajibika kugharamia matibabu yake wakati mtoto atakapougua akiwa shuleni.

**Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

- Wizi
- Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
- Kugombana na kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
- Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule, ila katika shule hii huruhusiwi kabisa kusuka nywele kwa mtindo wowote ule.
- Kufuga ndevu.
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.

- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati,Mahusiano ya jinsi moja,Ubakaji,kuoa au kuolewa.
- Kupata ujauzito au kutoa mimba.
- Kusababisha mimba.
- Kushiriki matendo ya uharifu,siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
- Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- Kudharau Bendera ya Taifa.
- Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
- Uharibifu wa mali ya umma kwa Makusudi.

.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Tumia nafasi hii muhimu ambayo Taifa limekupa upendeleo maalumu. Ufikapo shuleni jitahidi kusoma kwa bidii ili uiokoe familia yako pamoja na Taifa kwa ujumla.**

Nafasi uliyopewa ni mlango wa kuingia katika JAHAZI linalokuelekeza kwenye BANDARI ya mafanikio katika maisha.Inabidi uitumie nafasi hii kwa uangalifu ukiweka juhudi zako zote katika maelekezo utakayopewa hapa shuleni,iwe ndani ya darasa au nje.NIDHAMU, UTIIna USHIKIRIANO ni mambo muhimu yatakayo kuwezesha kufikia mafanikio haya.Unatazamiwa kutafuta MAARIFA kukuza TAALUMA,kutunza MAZINGIRA na kuwa MTIIFU.Mwisho napenda kukutakia maandalizi mema ya kujiunga na Shule ya Sekondari Nansimo.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

…………………………………..

**JUSTUS L. DEOGRATIAS**

**MKUU WA SHULE**

NB:

Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule 0769959007
- Makamu Mkuu wa Shule: 0757350240
- Mwandamizi Taaluma: 0755774100
- Mwandamizi Malezi 0762609999

**PMO – RALG**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

NANSIMO SEKONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 316,
**BUNDA.**
13 MAY, 2026

The Medical Officer,
………………………………………..
………………………………………..
………………………………………..

**RE**.........................................................................................**(Full Name of Student)**

Please kindly examine the above, named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.

- (a) Eye – sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech
  (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy
- Neurosis
- Pregnancy
- Other serious diseases

**PART B**

**<u>MEDICAL CERTIFICATE</u>**

(To be completed by a government Medical Officer)

I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNFIT or full time of schooling.

- Eye – sight ………………………………………………………………………
- Hearing ……………………………………………………………………...
- Limbs ……………………………………………………………………
- Speech …………………………………………………………………
- Venereal diseases ……………………………………………………
- Leprosy …………………………………………………………………
- Epilepsy ……………………………………………………………………………
- Neurosis ………………………………………………………………………………
- Pregnancy ……………………………………………………………………………
- Other serious diseases …………………………………………………………………

Date: …………………………………………… Signature: ………………………………

Station:……………………………………….. Designation: ……………………………

**SHULE YA SEKONDARI NANSIMO**

**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

- JINA KAMILI LA MWANAFUNZI: ______________________________________________
- TAREHE YA KUZALIWA: ________________________________
- KABILA : _______________________________
- DINI: ___________________________________
- SHULE ATOKAYO: ____________________________________________
- MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/ KIJIJI CHA _________________________
- KATA YA: _____________________________ TARAFA YA: ____________________
- WILAYA YA: ___________________________ MKOA WA:
- WAZAZI WOTE WAPO HAI.MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)
- JINA KAMILI MZAZI/MLEZI: ____________________________________________________
- KAZI YA MZAZI/MLEZI: _______________________KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO
- ANUANI YA MZAZI/MLEZI:_____________________________SIMU: _________________

**TAMKO LA MWANAFUNZI**

- Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.
- Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.
- Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Makongoro Sekondari. naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.
- Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.
- Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

**JINA LA MWANAFUNZI** **SAHIHI** **TAREHE**

_____________________________ ________________ ___________________

**FOMU YA AHADI YA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

JINA LA MZAZI/MLEZI: ________________________________________________

- Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya Sekondari Nansimo aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

- Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

- Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

- Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Nidhamu nzuri ya motto ndiyo mafanikio yake.

- Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo, fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** **TAREHE**

______________________________ ________________

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI**

______________________________________

**FOMU YA WAZAZI NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI WANAOWEZA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI SHULENI PAMOJA NA TAARIFA ZAO MUHIMU.**

**PICHA YA PASSPORT**

Jina la mzazi au ndugu ……………………………………..
Uhusiano na mwanafunzi……………………………………
Namba za simu: ………………………… Au ……………… Kazi ………………………………………………….
Mahali unapoishi : Mkoa wa ……………………
Wilaya ya ………….………
Kata ya …………….…….…………..
Mtaa/kitongoji cha……………………………...

**PICHA YA PASSPORT**

Jina la mzazi au ndugu ……………….……
Uhusiano na mwanafunzi…………………………………… Namba za simu: ........................................................ Au
Kazi : ……………………………………..……..
Mahali unapoishi : Mkoa wa ……….……………..
Wilaya ya ……………..…….………
Kata ya ……………….……….
Mtaa/kitongoji cha…………

**PICHA YA PASSPORT**

Jina la mzazi au ndugu ……………………………………………
Uhusiano na mwanafunzi…………………………………………
Namba za simu: ………………………… Au ………………….
Kazi : ……………………………………………..……...
Mahali unapoishi : Mkoa wa …………………………….……
Wilaya ya …………………….………
Kata ya ……………….….…………
Mtaa/kitongoji cha………

**PICHA YA PASSPORT**

Jina la mzazi au ndugu ……………………………………… Uhusiano na mwanafunzi……………………………………… Namba za simu: …………………. Au ………………………… Kazi : ………………………………………..……...
Mahali unapoishi : Mkoa wa ……………………………….……
Wilaya ya …………………….………
Kata ya ……………….….…………
Mtaa/kitongoji cha……………………

OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI NANSIMO

MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI/MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO/FUJO NA MAKOSA YA JINAI KATIKA SHULE YA SEKONDARI NANSIMO.

Mimi ………………………..wa kidato cha……….Tahasusi ya …………………mwaka ………….Naahidi kwamba katika maisha yangu ya uanafunzi katika shule ya sekondari Bunda sitashiriki katika mgomo wa aina yoyote ile na sitakataa adhabu itakayotolewa dhidi yangu kutokana na makosa nitakayotenda nikiwa mwanafunzi. Pia naahidi kutoshiriki au kusababisha fujo ya aina yoyote shuleni na sitashiriki kutenda makosa ya jinai, naahidi kusoma kwa bidii na kufuata sheria, taratibu na kanuni za shule

Sahihi ya mwanafunzi: ________________ Tarehe: _____________________

**AHADI/ TAMKO LA MZAZI KUHUSU MWANAFUNZI**

Mimi ___________________________Mzazi/mlezi wa mwanafunzi ________________________________wa kidato cha _______Tahasusi ya ________________mwaka ____________mwanangu hatashiriki migomo, fujo na wala makosa ya jinai kama yeye anavyoahidi nami ninaahidi kutoa ushirikiano kwa uongozi wa shule ili mwanangu aweze kutimiza na kufuata taratibu, sheria na kanuni za shule. Iwapo atakiuka taratibu, sheria na kanuni za shule hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi: __________Namba ya simu: ______________

Tarehe: ______________

# ORODHA YA VITABU

Mzazi/mlezi kumbuka kwamba, ili mwanafunzi aweze kufikia malengo yake ya kitaaluma, anapaswa pia awe anasoma vitabu. Unaombwa na Uongozi wa shule kumnunulia mwanao angalau kitabu kimoja kwa kila somo kulingana na masomo anayosoma (Vitakaguliwa siku ya kuripoti shuleni).

**HKL**

i)English for Advanced Secondary School Student's Book F5 (TIE)

ii) Kiswahili Kitabu cha Tano Kitabu cha Mwanafunzi (TET)

**Vitabu vya Riwaya/Tamthiliya na Mashairi**

01. Shujaa mirambo – Emmanuel Mbogo
02. Dunia uwanja wa fujo – Euphrazy Kezilahabi
03. Mukwava wa uhehe – M. Mulokozi
04. Usaliti mjini– Francis Imbuga
05. Ua la faraja – E. Mkufya
06. Mirathi ya hatari – C. G. Mung’ong’o

**The List of Readings for English Language, Advanced Level**

01. Animal farm – George Orwell
02. The horizon unveiled – Fellowes Mwaisela
03. The opportunist elite – Nyambori Nyangwine
04. The government inspector – Nikolai Gogoi
05. An enemy of the people – Henrik Ibsen
06. A taste of heaven – Farouk Topan

iii. History for Advanced SecondarySchools' Student's Book Form Five (TIE)

iv. Academic Communication for Advanced Secondary School Student's Book Form Five (TIE)

**EGM**

01. Physical Geography for Advanced Secondary Schools Student's Book (TIE)
02. Practical Geography for Advanced Secondary Schools Student's Book (TIE)
03. Micro Economics for Secondary School Student's Book (TIE)
04. Advanced Mathematics for Advanced Secondary School Student's Book (TIE)

**HGE**

01. Physical Geography for Advanced Secondary School Student's Book (TIE)
02. Practical Geography for Advanced Secondary School Student's Book (TIE)
03. Micro Economics for Secondary School Student's Book (TIE)
04. History for Advanced Secondary Schools Student's Book (TIE)

**CBG**

01. Biology for Advanced Secondary School Student's Book Form five (TIE)
02. Organic Chemistry for Advanced Secondary School Student's Book (TIE)
03. Physical Chemistry for Advanced Secondary School Student's Book (TIE)
04. Practical & Physical Geography for Advanced Secondary Schools Student's Book (TIE)
05. Basic Applied Mathematics for Advanced Secondary School Student's Book
06. Academic Communication for Advanced Secondary School's Student's Book Form Five (TIE)